

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L. P. 20,
MISUNGWI.

Simu: 255-732980745

Nukushi: 255 732980745

Barua Pepe: ded@misungwidc.go.tz

Tovuti: www.misungwidc.go.tz

14, Februari 2022

MISUNGWI

TAARIFA KWA UMMA

**YAH: ZOEZI LA UWEKAJI WA ANUANI ZA MAKAZI NA
POSTIKODI KATIKA VITONGOJI VYOTE VYA HALMASHAURI YA
WILAYA YA MISUNGWI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, anapenda kuwataarifu Wananchi wote wa Wilaya ya Misungwi na Watanzania kwa ujumla kwamba Halmashauri ya Misungwi itazindua rasmi zoezi la Uwekaji wa Anuani za Makazi na Postikodi (**POSTCODE**) siku ya Alhamis tarehe 17, Februari 2022 kuanzia Saa 2;00 asubuhi.

Zoezi la Uzinduzi wa Uwekaji wa Anuani za Makazi na Postikodi litafanyika katika Viwanja vya Soko Jipya la Mji wa Misungwi katika maeneo ya Kitongoji cha Bariadi ambapo Mgeni Rasmi atakuwa Mkuu wa Wilaya ya Misungwi na lengo la zoezi hilo ni kuweka namba za Makazi katika Kaya na uwekaji wa Vibao katika Mitaa na Barabara na baadaye uchukuaji na uwekaji wa taarifa sahihi za mmliki na tegemezi kwa kila Kaya kwenye mfumo wa Kielektroniki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Misungwi anawaomba Viongozi wa Chama na Serikali, Viongozi wa madhehebu ya Dini, Taasisi za Umma, Mashirika na Wadau wa Maendeleo na Watendaji wa ngazi zote pamoja na Wananchi wote kuijandaa kikamilifu na kutoa ushirikiano mkubwa katika kufanikisha zoezi hili'muhimu kwa ustawi wa Halmashauri ya Misungwi na taifa kwa ujumla.

Nawasilisha,

LEOKADIA HUMERA
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MISUNGWI
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MISUNGWI

NAKALA:-

- Mbao zote za Matangazo - Maeneo ya ofisi zote za Umma
- Tovuti ya Halmashauri - www.misungwidc.go.tz